Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | July-2022

EAJK

# Muainisho wa Matamko Tendi katika Riwaya za Ken Walibora

**Authors**
**Koko A. Monica [1]; Juliet A. Jagero [2]; Naomi N. Musembi [3]**
**Main author email:** kmonica086@gmail.com

**(1.2.3) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Koko, A. M., Jagero, J. A., & Musembi, N. N. (2022). Muainisho wa matamko tendi katika riwaya za Ken Walibora. *Eastern Africa journal of kiswahili,* 1(1), 16-25. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.82

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 08.05.2022
Accepted: 11.06.2022
Published: 31.07.2022

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2022 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Makala hii inanuia kuchunguza matamko tendi yanayopatikana katika dayolojia baina ya wahusika katika riwaya za Walibora. Madhumuni mahsusi ni kuainisha MT yaliyotumiwa katika riwaya za Walibora. Makala iliongozwa na Nadharia ya Vitendo Usemi. Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa huku taaluma ikiwa ni pragmatiki. Sampuli dhamirifu ilitumika kuteua riwaya nne za Walibora huku sampuli dabwadabwa ikitumika kuteua MT kutoka riwaya hizo. Mbinu ya unukuzi ilitumiwa kudondoa sehemu za matini na kuwekwa kwenye jedwali la matukio. Deta zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kulingana na madhumuni ya makala na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali. Makala ilionyesha MT mengi kuwa MTE yakiwa 121 kwa 285. Idadi kubwa ya MT yalikuwa ya kuamuru kumaanisha msemaji alitumia mamlaka aliyo nayo kushrutisha msemewa atende jambo kwa kuzingatia kanuni ya kiilokusheni. Mengine yakiwa ya kukaribisha. Uchanganuzi wa MT una umuhimu katika usomaji, uchanganuzi na ufasiriaji wa mazungumzo ya wahusika na maana anayonuia mwandishi wa riwaya.

**Maneno muhimu:** Muainisho, matamko tendi, riwaya.

**UTANGULIZI**

Matamko tendi (MT) yamekuwa na mwamko mkuu katika falsafa ya lugha na isimu kwa sababu ya mvutano maalum unaodhihirika baina ya Semantiki na Pragmatiki (Harnish, 2007). Wasomi wamebeta kutoka mtazamo wa awali wa kifalsafa uliokuweko kuwa lugha ilikuwa tu chombo cha kueleza ukweli au uongo. Tetesi zilikuwa kwamba lugha ama ilisema ukweli au uongo. Austin (1962) anasema lugha ni zaidi ya hayo. Badala ya kueleza ulimwengu, yeye alidai kuwa lugha ilitekeleza vitendo katika ulimwengu. Kitenda ni kauli ambayo, licha ya kueleza kitendo, wakati huo huo hukitenda kitendo hicho (Bennett & Royle, 1995; Huang, 2009). Matamko tendi ni vitendo vinavyotekelezwa kwa kuvitamka tu kwa sauti. Hutumiwa kutekeleza jambo kuliko kusema kitu kilivyo au sivyo. Hutangulizwa kwa kiambishi kinachodhihirisha kutokuwepo utata nguvu ilokusheni zake (Leech, 1987; Blakemore, 1992; Levinson, 1983). Lyons (1977) anaeleza MT bainifu kuwa aghalabu huwa na maana bayana kuliko MT ya kimsingi. Chambilecho pragmatiki ni ufasiri wa kile watu humaanisha katika muktadha maalum na namna muktadha huathiri kinachosemwa (Yule, 1996).

Makala hii inatambua kuwa Vitendo usemi (VU) havitokei tu katika mazungumzo ya ana kwa ana bali pia katika dayolojia katika riwaya na hivyo huakisi uhalisia wa maisha. Ni muhimu kutaja hapa kwamba uchanganuzi wa VU katika matini ya riwaya haujapewa kipaumbele (Akinkurolere & Ariyo, 2015). Nadharia ya VU kwa muda mrefu haijatiwa kwenye ramani ya Isimu ya Kiswahili (Kyeu, 2014). Si watafiti wengi wamewahi kutumia nadharia za kiisimu kuchunguza fasihi. Makala hii ni ufafanuzi wa matumizi ya nadharia ya kiisimu ya VU katika uchanganuzi wa dayolojia katika riwaya za Walibora.Makala inanuia kuainisha aina mbalimbali za MT kwa kutazama vitendo usemi ilokusheni (VUI) vinavyojitokeza katika kauli za wahusika. Aina za MT yatakayojadiliwa yalitokana na aina mbalimbali za VUI. Vitendo ilokusheni ambavyo ndivyo vitendo halisi vinavyotekelezwa katika harakati za kutamka maneno ndivyo msingi wa nadharia ya VU.

Kisemantiki, vitendo ilokusheni ndiyo NI ya tamko yaani maana yake halisi inayokusudiwa (Austin, 1962). Ni kupitia mtazamo huu ndio makala hii iliangazia MT na NI katika riwaya hizi nne. Hivi ni kusema kuwa kila aina ya vitendo ilokusheni kutoka kila kauli ya mhusika vinatumiwa kuwasilisha kusudi kamili la msemaji ambavyo pia vitamsaidia msomaji kuelewa wanachomaanisha wasemaji na mwandishi. Tafiti zilizochunguzwa kwa nadharia ya VU ziliangazia aina za VUI pekee (Oloo, 2019). Si kazi nyingi zimeshughulikia MT katika riwaya. Makala hii ilinuia kujaza pengo hilo kwa kuchunguza muainisho wa MT katika dayolojia kama mkakati wa kuendeleza maudhui. Nadharia hii ina umuhimu mkubwa katika kuchunguza maana kwa misingi ya kiisimu.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Austin alitambua makundi matano ya VUI. Ameyaainisha makundi haya kwa misingi ya athari za kiutendaji. Akizingatia vitenzi vya kiilokusheni, Austin (1962) ameainisha VUI kuwa maamuzi, amri, ahadi, hisia na vifunuzi. Kwa upande mwingine Searle (1969) anaonelea kwamba kigezo muhimu katika kuainisha VU ni ilokusheni. Kwake ilokusheni ni kisawe cha VU. Baadaye Searle alidai kwamba muainisho wa Austin haudhihirishi bayana tofauti iliyopo kati ya vitenzi tendaji na vitendo vyenyewe. Pia ufafanuzi anaotoa Austin ni pana mno. Mfumo ambao makala hii ilirejelea ni mfumo wa Searle (1986, 1989) unaoweza kurejelewa kama wa kisasa na unaoegemea ulimwengu halisi. Pia, muainisho wa Searle una uwiano na muamano mzuri kuliko ya Austin. Lengo kuu la makala hii ni kuzalisha uainishaji wa MT. Hivyo basi, mshawasha wa wanaisimu na wanafalsafa unafaa kuelekezwa kwenye kipengee cha ilokusheni katika lugha kuliko mgawanyo baina ya vitendo usemi lokusheni (VUL) na VUI (Leech, 1983; Bach & Harnish, 1979). Mfumo wa Searle ulifaa katika uainishaji VUI mbalimbali vilivyomo kwenye matini zilizoteuliwa.

Makala hii ilihusisha nadharia ya VU (Searle, 1969). Nadharia ya VU iliasisiwa mwaka wa 1962 na mwanafilosofia John Langshaw Austin kupitia mihadhara yake aliyotoa na kuchapishwa baadaye yakiwa na kichwa "Jinsi ya kutenda kwa kutumia maneno." Nadharia hii huchunguza jukumu la matamko kwa kuyahusisha na tabia ya msemaji na msemewa. Yule (1996) anasema VU hushughulikia nia ya kimawasiliano ya msemaji katika kutamka. Mihimili ya nadharia hii ni kuchunguza matini kwa mkabala wa VU, nia ya msemaji huwa ni jambo muhimu. Pasi kuielewa nia ya mwandishi, kipashio cha kiisimu hakina maana yoyote ya kudumu (Patte, 1988). Kuvielewa VU huhusisha ufahamu wa muktadha. Muktadha wa tamko hudokeza msingi wa maana ya tamko lenyewe (Austin, 1962). Lengo la kimsingi la kusema ni kuwasilisha nia (Bach & Harnish, 1979). Upo utegemeano baina ya msemaji, msemewa na tamko. Ni muhimu kuzingatia lengo la kutamka. Hili huwa ni msemewa kufasiri na kutekeleza

vilivyo tamko (Bach & Harnish, 1979; Malik, 1995). Watu hutumia lugha wakiwazia hadhira yao (Nyangeri, 2014). Mihimili hii ya nadharia ya VU ilitumiwa kueleza muainisho wa MT na kueleza maana dhamirifu kwa kuangalia utegemeano baina ya msemewa, msemaji na tamko.

Searle (1969; 1979; 1986) alijaribu kuainisha VUI tena kwa vipengele 12. Makala hii iliziangazia baadhi ya vigezo hivyo. Vigezo vya kutimizwa ili kufaulu kwa MT ni kama vifuatavyo; Hoja ya kiilokusheni au jukumu la tendo, kama vile kusababisha mtu kutenda jambo kama kuamuru, kuuliza ili kupata jibu: Welekeo wa ufaafu/ uhusiano kati ya neno na ulimwengu kama unavyoelezwa kwa njia tofauti na vitendo mbalimbali; Kanuni ya uaminifu au hali ya kisaikolojia. Kama vile imani, matarajio, azimio na matakwa; Nguvu ilokusheni inayotumiwa kutamka matamko. Kwa mfano, kuapa na kukisia; Mamlaka ya mzungumzaji na msemewa kama vile kuomba ama kuamuru; Matamko mengine kuhitaji muktadha maalumu au taasisi nje ya kiisimu. Muktadha uwe unafaa kwa kitendo hicho kufanyika. Mwisho, Vitambulisho VU na vitambulisho vya kisarufi. Kwa kuzingatia vigezo hivyo makala hii iliibusha aina tano za MT. Kazi hiyo inachangia makala hii kwani makundi haya ndiyo yaliyozingatiwa katika makala hii katika kugawa MT. Makundi hayo ni matamko tendi taarifa, hisia, vielekezi, ahadi na maamuzi.

## MATOKEO YA UTAFITI

Aina za MT yaliyojadiliwa yalitokana na aina mbalimbali za VUI. Katika uchanganuzi, mtafiti alionyesha deta iliyokusanywa na kuainishwa kulingana na muainisho wa Searle (1979) wa VUI. Mtafiti ametumia vifupisho na nambari ili kuonyesha aina ya tamko. Riwaya zilirejelewa kama *Kidagaa Kimemwozea, Kufa Kuzikana, Ndoto ya Almasi na Siku Njema.* Aina za MT yalirejelewa kama **MTA**- Matamko tendi ya Ahadi, **MTE**- Matamko tendi Vielekezi, **MTH**- Matamko tendi ya Hisia, **MTM**- Matamko tendi Maamuzi, **MTT** -Matamko tendi Taarifa. Hivyo basi, riwaya: aina ya MT: nambari. Uchanganuzi wa deta 285 ulionyesha kuwa kulikuwa na MTE 121 idadi iliyo kubwa zaidi, ikifuatiwa na MTH 82, MTM 32, MTA 29 na mwisho ni MTT 21 katika riwaya za Walibora. Muhtasari wa idadi ya MT katika riwaya zote umewekwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 1: Muanisho wa MT katika Riwaya za Walibora**

| AINA ZA MT | *Siku Njema* | % | *Kufa Kuzikana* | % | *Ndoto ya Almasi* | % | *Kidagaa Kimemwozea* | % | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MTE** | **21** | 17 | **35** | 29 | **31** | 26 | **34** | 28 | **121** | 42 |
| **MTH** | **25** | 30 | **19** | 23 | **12** | 15 | **26** | 32 | **82** | 29 |
| **MTM** | **1** | 3 | **10** | 32 | **8** | 23 | **13** | 42 | **32** | 11 |
| **MTA** | **4** | 14 | **7** | 31 | **9** | 28 | **8** | 28 | **29** | 11 |
| **MTT** | **2** | 5 | **3** | 14 | **6** | 24 | **10** | 57 | **21** | 7 |
| **Jumla** | **53** | | **74** | | **66** | | **91** | | **285** | |

Kulingana na uchanganuzi huu wahusika katika riwaya zilizotafitiwa kupitia matamko yao walionyesha hali kamili za kisaikolojia au uaminifu, waliwasilisha hali ilivyo, walionyesha hisia zao kutokana na hali zilizoko, kujitolea kutekeleza wajibu fulani katika wakati ujao, kusababisha wasikilizaji wao kutenda vitendo fulani na pia kujaribu kubadilisha ulimwengu kupitia matamko yao. MT licha ya kuwa na sifa za kijumla, yana sifa maalumu zinazobainisha tofauti kati ya aina hizi tano za MT.

### Muanisho wa MT katika Riwaya

Makala hii ilizingatia vigezo saba ili kuibuka na makundi matano ya MT. Searle (1989) alitoa vigezo vya kutimizwa ili kufaulu kwa VU kama ifuatavyo; Hoja ya kiilokusheni au jukumu la tendo, welekeo wa ufaafu/ uhusiano kati ya neno na ulimwengu, baadhi ya VU vinahitaji uproposisheni kwa kiwango fulani, kanuni ya uaminifu au hali ya kisaikolojia, nguvu ilokusheni inayotumiwa kutamka matamko, mamlaka ya mzungumzaji na msemewa na matamko

mengine huhitaji muktadha maalumu au taasisi nje ya kiisimu. Makala ilibainisha makundi yafuatayo ya MT; kuamuru yalitoka katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* ambayo yalikuwa 8 yakiwakilisha asilimia 44 huku riwaya ya *Siku Njema* ikiwa na idadi ya chini zaidi ya 2 ambayo ni asilimia 11. Matamko mengi ya kuuliza yalitoka katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 6 ambayo ni asilimia 43. Kwa ujumla MTE yalibainishwa zaidi katika riwaya ya *Kufa Kuzikana* ambayo yalikuwa 35. Hii inawakilisha asilimia 29 yakifuatiwa na riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 34 ambayo ni asilimia 28. Kwa jumla uchanganuzi ulionyesha idadi kubwa ya matumizi ya kuamuru 18, kuuliza 14, ikifuatiwa na kukumbusha 11, kusihi 11, kuomba 10, kushauri 10 miongoni mwa mengine. Maelezo ya kina yameonyeshwa katika jedwali lifuatalo;

**Matamko Tendi Vielekezi (MTE)**

MTE ni MT ambayo msemaji hujaribu kumfanya msemewa kutenda jambo kwa kutaja kile anachokitaka msemaji (Searle, 1969). MTE yanaweza kusemwa kiungwana ama kwa ukali. Sifa zinazotenga kikundi cha MTE, aghalabu, sharti tamko liwe la hiari na kwa wakati ujao. Uhusiano ni wa neno- ulimwengu. Pia msemaji huwa na matarajio. Aina mbalimbali za MTE yalijadiliwa (Wunderlich, 1980).

Makala ilibaini MTE 121 ambayo ni asilimia 42 katika riwaya zote zilizoteuliwa. Katika kikundi hiki matamko yaliyokuwa na idadi ya juu zaidi yalikuwa ni kuamuru ambayo yalikuwa 18 au asilimia 15 yakifuatiwa na matamko ya kuuliza ambayo yalikuwa 14. Hii inawakilisha asilimia 12. Matamko mengi ya

**Jedwali 2: Muanisho wa MTE katika Riwaya**

| MTE | *Siku Njema* | % | *Kufa Kuzikana* | % | *Ndoto ya Almasi* | % | *Kidagaa Kimemwozea* | % | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuamuru | 2 | 11 | 3 | 17 | 8 | 44 | 5 | 28 | 18 | 15 |
| Kuuliza | 2 | 14 | 2 | 14 | 4 | 29 | 6 | 43 | 14 | 12 |
| Kukumbusha | 2 | 18 | 2 | 18 | 3 | 27 | 4 | 36 | 11 | 9 |
| Kusihi | 3 | 27 | 4 | 36 | 2 | 48 | 2 | 48 | 11 | 9 |
| Kuomba | 2 | 20 | 3 | 30 | 1 | 40 | 4 | 40 | 10 | 8 |
| Kushauri | 0 | 0 | 2 | 20 | 4 | 40 | 4 | 40 | 10 | 8 |
| Kusali | 2 | 29 | 3 | 43 | 1 | 14 | 1 | 14 | 7 | 6 |
| Kuonya | 2 | 29 | 1 | 14 | 3 | 43 | 1 | 14 | 7 | 6 |
| Kuita | 1 | 20 | 1 | 20 | 1 | 20 | 2 | 40 | 5 | 4 |
| Ruhusu | 1 | 25 | 0 | 0 | 2 | 50 | 1 | 25 | 4 | 3 |
| Kusisitiza | 2 | 50 | 0 | 0 | 1 | 25 | 1 | 25 | 4 | 3 |
| Kurai | 0 | 0 | 4 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 3 |
| Kuagiza | 0 | 0 | 1 | 50 | 0 | 0 | 1 | 50 | 2 | 2 |
| Himiza | 0 | 0 | 2 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kukemea | 0 | 0 | 2 | 67 | 1 | 33 | | 0 | 0 | 2 |
| Kuamini | 1 | 50 | 1 | 50 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kualika | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 100 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Pendekeza | 0 | 0 | 1 | 100 | 0 | | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Shutumu | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 1 | 100 | 1 | 1 |
| **Jumla** | **21** | **47** | **35** | **29** | **31** | **26** | **34** | 28 | 121 | 43 |

Mifano ya MTE ni kama ifuatayo;
***Siku Njema*: MTE: 11**"*Alice please shut up!" alifoka mama mtu. "Can you stop that nonsense! Huoni kuwa huyu mtu ni mgonjwa. Ingia ndani umshikilie tumpeleke hospitalini." Akaamuru mama mtu. Alice akasalimu amri shingo upande*. Uk 108

Alice na mamake walikuwa mkahawani ambapo Kongowea pia alikuwa akinywa chai ya mkandaa katika mji wa Kitale, Makutano kwa Ngozi. Kongowea akawa mgonjwa wa malaria na kuanza kutapika mkahawani. Mama mtu akataka kumsaidia naye Alice akakataa kwamba haendi na mtu huyo. Mama analazimika kumwamuru Alice. MT hapa ni kuamuru. Yaani msemaji anamtarajia msemewa kufanya kitendo fulani la hiari na ni kwa wakati ujao. Mama ana matarajio kwamba akimsaidia mgonjwa huyu atapata kupona. Alice aliyeghadhabika akakubali shingo upande kumshikilia mgonjwa awekwe garini.

***Siku Njema*: MTE: 15** *"Nakuombeni mniruhusu kukivua kilemba cha umalenga na ubingwa wa Kiswahili."* Uk 127

Kongowea anaomba asipewe sifa nyingi na wanafunzi wa Suwerwa. Anaomba apewe ruhusa ya kuvua sifa za ubingwa wa Kiswahili. Huu ni wakati Bi. Nambuye Pilipili alipomwalika kuja kuzungumza na wanafunzi shuleni kuhusu Kiswahili. MT ni kuomba na kuruhusu. Hali ya wingi katika na –ku- omb- e-ni. Sifa ya urejelezi pia imetumiwa katika nakuombeni. Mbali na sifa hizi za kijumla, kuna sifa bainifu za MTE. Msemaji anamfanya msemewa kutenda jambo ambalo ni kuhurusu avue kilemba cha umalenga. Tendo hilo liwe la hiari na la kutendwa wakati ujao. Ni jukumu la wanafunzi kukubali jambo hilo au la. MT tayari limetokea sawia na tamko hilo. Kwa hivyo welekeo wa ufaafu ni neno-ulimwengu.

***Kufa Kuzikana*:MTE:29** *"Wakanju ni mbwa tu."*

*"Eech! Tamari wacha matusi hapa. Usinizulie zani bure," Tim alimsihi dadake.*

*"Wendapi Akida? Rudi bwana," alinisihi.*

*" Niache nende shemeji." Hasira zilinipanda nikaanza kutetemeka.* uk 130

Tamari anamtusi Akida kwamba Wakanju ni mbwa tu.Tim anamsihi dadake Tamari asimtusi rafikiye. MT iliyotumiwa ni kusihi. Tamari alidanganya nduguye kwamba usiku wa kuamkia leo, Akida alijaribu kumbaka. Jambo hilo linamuudhi sana Akida ikichukuliwa kuwa ni Tamari ndiye aliyekwenda kumsumbua usiku na akamkataza. Alijichomoza nje ili kutokomea mbali. Tim anamfuata nje ili kumrudisha ndani wasuluhishe mambo hayo. Akida alisema hajawahi kuumbuliwa na mtu namna hiyo. Tim alimsihi lakini akatokomea kwenda Sangura. Msemaji Tim anajaribu kumfanya msemewa Tamari atende jambo la kutozua vurugu na ni kwa hiari yake. Tendo litendwe kwa wakati ujao na Tim ajue chanzo cha matusi hayo.

**Matamko Tendi Hisia (MTH)**

Katika aina hii ya MT, msemaji huwasilisha hali yake kisaikolojia kupitia proposisheni. MTH huzingatia hisia na mielekeo ya mtu. MP ni jambo linalowaathiri msemaji au msikilizaji. MTH hayana welekeo wa ufaafu wa upande wowote kwa sababu proposisheni hujitokeza kwa uchukuliaji wala haitangazwi (Searle, 1989). (Kaburise, 2011; Umar, 2016; Searle, 1979) waliorodhesha mifano ya VUH. Uchanganuzi ulionyesha kuwa kulikuwa na MTH 82 katika riwaya za Walibora. Uchanganuzi ulionyesha idadi kubwa ya matumizi ya kukaribisha 18, kuomba radhi 14, kuliwaza 13, kushukuru 13, kusalimu 7, kupongeza 7, kusikitika 6, kujuta 2 na kuhurumia 2.

Makala ilibainisha MTH 82 ambayo ni asilimia 29 katika riwaya zilizochunguzwa. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ni *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 26 ambayo ni asilimia 32. Hii ilifuatwa na riwaya ya *Siku Njema* ikiwa na idadi ya 25 ambayo ni asilimia 30. Aina ya MT yaliyokuwa mengi ni kukaribisha ambayo yalikuwa 18 yakiwa ni asilimia 22. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ndiyo iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kukaribisha yakiwa ni 6 ambayo ni asilimia 33. Idadi iliyokuwa ya chini zaidi ni riwaya ya *Kufa Kuzikana* ambayo yalikuwa 2. Hii inawakilisha asilimia 11. Aina ya pili katika idadi ya juu katika MTH yalikuwa matamko ya kuomba radhi yakiwa 14 ambayo ni asilimia 17. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kuomba radhi ni Kidagaa *Kimemwozea* yakiwa ni 6 ambayo ni asilimia 43. Mifano ya MTH ni kama ifuatayo;

***Ndoto ya Almasi*: MTH: 08** *"Karibu mwanangu," alimwambia mwanawe. "Nenda ndani umsalimu babako."*

*"Kichana," Mzee Masasi aliita kwa utani. "Wapi sigara yango?" alimnyoshea mkono wakasalimiana huku wanaangua vicheko.*

*Almasi alitoa pakiti ya sigara chapa ya 'sm' akamkabidhi.* uk109

Almasi pamoja na umbu wake wameitwa nyumbani. Babake Masasi hapo mbeleni alikuwa amemfukuza kwamba akirudi asimpate huyo jambazi humo. Hata alikataa kumsalimia kwani alitiwa jela. Masasi

akamkana kuwa mtoto wake. Sasa Masasi ni mgonjwa: alianguka alipolewa na akachomwa mguu kwa kijiti. Mama alipomwona Almasi amerudi akamkaribisha nyumbani na kumshauri aingie ndani kumsalimia babake. MT hapa na kukaribisha na kusalimu. Masasi alifurahi sana kumwona mwanawe kwa vile alijua atamfaidi kwa kumletea sigara ndiposa anamwuliza 'wapi sigara yango? Akanyoosha mkono na kumsalimia kwa furaha. Katika hali hiyo proposisheni haitajwi bali msemaji na msemewa wote wanaathiriwa. Msemaji anaonyesha hali ya kisaikolojia na hisia na mielekeo yake. Matamko hayana ufaafu wa upande wowote. Msemewa anachukulia kwamba kwa sababu ya hali ya babake amesamehewa ndiposa wanacheka na anatoa sigara ya sm na kumpa. MT hapa ni kukabidhi.

**Matamko Tendi Maamuzi (MTM)**

Searle (1989) anaeleza MTM kuwa ni aina ya VU ambavyo, ikiwa vitafaulu kutendwa, matokeo yake ni upatikanaji wa proposisheni iliyotamkwa kama athari ya kutamkwa kwake tu. Kwa mujibu wa Searle (1965), MTM ni VU vya msemaji kubadilisha ulimwengu kupitia maneno. Hivi hudhihirisha hatua andamizi iliyochukuliwa na msemaji baada ya kutoa tamko. Kwa mfano, 'umefutwa kazi.' ikitamkwa na mtu anayefaa, wakati unaofaa na mahali panapostahili (Bussmann, 1996). Welekeo wa ufaafu ni kwamba utekelezaji wa uamuzi huleta ufaafu wenyewe tendo linapotimilika. MTM hujaribu kuelekeza lugha kuwiana na ulimwengu ila hayajaribu kufafanua hali ilivyo. Baadhi ya MTM huingiliana na MTT. Katika taasisi nyingine mamlaka yatahitajika ili kufanya uamuzi fulani kama vile hakimu (Sadock, 1974; Searle, 1989).

Uchanganuzi ulionyesha idadi kubwa ya matumizi ya kupa jina 7, kutia nguvuni /hukumu 7. kumpata mshtakiwa na kosa/ maamuzi 5, kutangaza 4, kuachiliwa 3, piga marufuku 2 kuachisha mwajiriwa kazi 2, kuteua 1, kuunga mkono kumbukumbu za mkutano 0, kuahirisha kikao 1, kubatiza 0, kuweka dau 0, kupa talaka 0 na kutangaza vita 0.

Makala ilibainisha MTM 32 ambayo ni asilimia 11 katika riwaya zilizochunguzwa. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ni *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 13 ambayo ni asilimia 42. Riwaya iliyokuwa na idadi ya chini zaidi ni riwaya ya Siku *Njema* ikiwa na idadi ya 1 ambayo ni 3%. Aina ya MT yaliyokuwa mengi ni kuhukumu ambayo yalikuwa 7 yakiwa ni asilimia 23. Riwaya ya *Kufa Kuzikana ndiyo* iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kukaribisha yakiwa ni 3 ambayo ni asilimia 43. Idadi iliyokuwa ya chini zaidi ni riwaya ya *Siku Njema* ambayo haikuwa na tamko la kuhukumu. Aina ya pili katika idadi ya juu katika MTM yalikuwa matamko ya kumpa jina yakiwa 7 ambayo ni asilimia 23. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kumpa jina ni Kidagaa *Kimemwozea* yakiwa ni 4 ambayo ni asilimia 57. Riwaya ya *Ndoto ya Almasi* ikawa na MT 3 ambayo ni asilimia 43. Mifano ni kama ifuatayo,

***Kufa Kuzikana*:MTM: 04** " *Rafiki yangu nimepigwa kalamu kazini."*
*'Makubwa."*
*Basi ameniuliza jana nilikuwa wapi ...unaisaliti kabila lako. Unamweka Mkanju nyumbani mwako Shauri Moyo?' .."Hebu toka hapa. Nimekufuta kazi."*
" *Basi ndio unaniona naja mapema hivi."*uk 65

Tim alikosa kwenda kazini ili kuhudhuria sherehe ya kuzawadiwa rafiki yake Akida. Ilikuwa sherehe ya kitaifa ya kuwatuza wanafunzi watatu bora nchini katika mtihani wa darasa la nane. Akida alikuwa wa tatu. Pam na Tim wakampeleka. Keshoye Tim alipoenda kazini ambapo ameajiriwa na mjomba wake, aliulizwa kwa nini anaishi na Akida ambaye ni Mkanju. Kwa sababu hizo akapigwa kalamu na mjomba wake. MT hapa ni kufutwa kazi. Ili mtu kufutwa kazi msemaji lazima awe na mamlaka ya kufanya hivyo. Hivi ni kusema kwamba alifutwa kazi na mwajiri wake. Taasisi nje ya muktadha wa kiisimu inahitajika. Muktadha hapa ni kazini. Tokeo la kutamkwa tendo ni kuwa sasa Tim hana riziki tena kwa kusema tu' nimekufuta kazi. Msemaji ameleta mabadiliko katika ulimwengu kwani ilibidi Tim kuuza baadhi ya vifaa vya nyumbani kama runinga ili kuendelea kuishi na kuikimu familia ya watatu. Hakuna hisia zinazowasilishwa kwani aliyefuta kazi ni mwajiri ilhali aliyefutwa ni mfanyakazi.

***Kidagaa Kimemwozea*: MTM:05** "*Sasa basi," aliendelea Mheshimiwa Mtemi. "Kwa vile uliletewa mtoto huyu, wewe ndiye babake. It is a straight forward case. Kachukue mwanao ukamtunze."*uk 41

Mtemi Nasaba Bora ameletewa mtoto na Amani. Mtoto alitupwa usiku mlangoni pa Amani. Ilipofika asubuhi Amani alimleta katika nyumba ya Mtemi. Mtemi akamwuliza kama amemwona na mimba kisha akaamua Amani amchukue mtoto na kuendelea

kumtunza. MT ni uamuzi. Ili tendo la uamuzi ufanywe lazima kuwe na taasisi nje ya kiisimu. Kuwa mtemi kunamweka msemaji katika hali ya kuweza kuamua kesi. Hakuna hisia zozote za kibinafsi wakati wa kufanya maamuzi. Hii ndiyo sababu Bi Zuhura anamwonea Amani huruma ilhali mtemi anaangalia hoja zilizoko. Sharti msemaji awe na mamlaka ili kufanya uamuzi. Nasaba ana cheo cha utemi. Welekeo wa ufaafu ni kwa pande zote mbili. Mtemi anasababisha mabadiliko katika ulimwengu wakati uu huu huwakilisha mambo yalivyo kwamba mtoto amepatikana lazima kuwe na mwenyewe. Hapa ndipo MTM huwiana na MTT.

***Kufa Kuzikana*:MTM: 09**"*Mwisho napenda kutaja kuwa mwathiriwa mwenyewe Tito Tembo yuko hapa kortini. Amezungumza nami kimbele na kunitaka niombe korti itupilie mbali kesi hii.*"

*" Nilikuwa na hasira. Naomba radhi.'*

*"Umeachiliwa nenda, lakini usirudie," alitoa kauli hakimu.*

*Nikatoka. Nilikuwa na mseto wa hisia zisizoeleweka*. Uk 193

Akida alipiga mtu kwa hasira kwa kudai jinsi alivyowaua Wakanju wengi. Aliyejitapa huyo alikuwa Tito Tembo naye Akida akadhani ni babake Tim. Alitoroka hadi Sangura. Baada ya miaka mitatu alirudi kujisalimisha kwa polisi. Kesi iliposikizwa ikagunduliwa kuwa babake Tim alijitia kitanzi mwenyewe na Tito Tembo hakuwa amefariki. Akida akaomba msamaha kuwa alikuwa na hasira. Tito akaomba kuachilia kesi hiyo. Korti ndiyo muktadha maalumu. Hakimu ndiye ana cheo cha kuachilia kesi. Kwa kutaja tu kwamba 'umeachiliwa' Akida anapewa nguo zake na kuondoka kortini kwa sasa yuko huru. Mabadiliko yanatokea ulimwenguni. Akida kutembea huru, kesi imekwisha. Tim kumchukua na kwenda naye nyumbani.

**Matamko Tendi Ahadi (MTA)**

MTA ni matamko ambayo huonyesha nia ya msemaji kutenda jambo fulani. MTA humdiriki msemaji kwa utendaji wa wakati ujao wa jambo lililomo kwenye proposisheni ya tamko lake (Bussmann, 1996; Searle, 1969). Katika aina hii ya MT, msemaji hujihusisha na utendaji wa kitendo. Hivi hujishughulisha na utoaji ahadi. Dhamira huwa ni kwamba msemaji huwa amejitolea kutekeleza wajibu fulani. MTA, kama MTE, huwa ya hiari na ni ya wakati ujao. Upande wa uhusiano ni kutoka ulimwengu kuelekea neno. Hali ya kisaikolojia ni matarajio. Aina za MTA zimeorodheshwa na (Levinson, 1983; Searle, 1989; Leech, 1983).

Uchanganuzi ulionyesha idadi kubwa ya matumizi ya kutisha 8, kubali 6, kuahidi 5, kuapa 4, dhamini 0, kupa 1, kukataa 1, kuhakikisha 2, kujitolea, kulaani 1, weka rehani na kutabiri 1.

Makala ilibainisha MTA 29 ambayo ni asilimia 11 katika riwaya zilizochunguzwa. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ni *Kufa Kuzikana* yakiwa ni 9 ambayo ni asilimia 31. Riwaya ya *Siku Njema* ikiwa na idadi ya chini zaidi 4 ambayo ni asilimia 14. Aina ya MT yaliyokuwa mengi ni kutisha ambayo yalikuwa 8 yakiwa ni 28%. Riwaya ya *Kufa Kuzikana* ndiyo iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kutisha yakiwa ni 4 ambayo ni asilimia 50. Idadi iliyokuwa ya chini zaidi ni riwaya ya *Siku Njema* na Ndoto *ya Almasi* ambayo yalikuwa 1 kwa asilimia 13. Aina ya pili katika idadi ya juu katika MTA yalikuwa matamko ya kukubali yakiwa 6 ambayo ni asilimia 21. Riwaya zote zilikuwa na idadi 2 ya matamko ya kukubali isipokuwa *Siku Njema.* Kwa mfano,

***Kidagaa Kimemwozea*: MTA: 01** "*Hata hivyo, tukija tukawa tutakukumbuka bila shaka."Aliahidi Amani.*uk 10

Amani na Imani walikuwa na mazungumzo marefu mwishowe DJ anawataka wamwahidi kuwa siku moja wakijaliwa kuwa matajiri wamkumbuke. Amani kwa hakika anaahidi kumkumbuka DJ atakapokuwa tajiri. MT hapa ni kuahidi. Msemaji hujihusisha na utendaji wa kitendo. Tendo ni hiari na ni wakati ujao. Hii inaonyesha nia ya msemaji. Hali ya saikolojia ni matarajio. Kwa kawaida ni tendo ambalo msemaji hangekitenda. Amani anaonyesha kuwa si rahisi wawe matajiri hata hivyo iwapo watakuwa, basi watamkumbuka DJ.

***Ndoto ya Almasi*: MTE: 20** "*We Nyamaza nimalize." Alifoka Tulienge kwa sauti kubwa ya kutisha.*uk 95

Wanafunzi walikuwa wamepiga mawe basi la mawingo. Tulienge akiwa mmoja wao anawasimulia wenzake namna vurugu ilivyoanza na namna aliukusanya umati mkubwa kwenda kumwokoa mwenzao. Mmoja wao alimkatisha ulimi alipokuwa akisimulia kisa hicho. Kisha anamtisha kunyamaza kwa sauti kubwa. MT hapa ni kutisha. Tendo ni la hiari na wakati ujao.

**Matamko Tendi Taarifa (MTT)**
Haya ni matamko yawasilishayo hali ilivyo. Kwa hivyo, huonyesha imani ya msemaji kuhusu tamko lake (Bussmann, 1996; Mathews, 2007). Hivi huonyesha kiwango alichojitolea msemaji kutekeleza aliyosema. Katika kutoa tamko la aina hii, msemaji huwakilisha ulimwengu kwa namna anavyoamini ulivyo. Kwa njia hii, anayafanya maneno yake kuoana na ulimwengu wake wa imani. Hii ina maana kwamba welekeo wa ufaafu wa MTT huwa neno-kwa-ulimwengu, kwa kuwa maelezo hulengwa yawiane na hali ilivyo ulimwenguni. Hali ya kisaikolojia ni imani. Kwa mfano, kiwango cha kuthibitisha huwa cha juu huku cha kubashiri huwa cha muda tu. Uchanganuzi ulionyesha idadi kubwa ya matamko ya kuarifu 5, kudai 5, kulalamika 2, kuthibitisha 1, kueleza 1, kutaja, kufafanua, kupambanua, kuambia 2, kukadiria, kuhitimisha 4, kufahamisha, kusadikisha, na kuringa 1.

Makala ilibainisha MTT 21 ambayo ni asilimia 7 katika riwaya zilizochunguzwa. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ni *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 12 ambayo ni asilimia 57. Riwaya iliyokuwa na idadi ya chini zaidi ni ya *Siku Njema* ikiwa na idadi ya 1 ambayo ni asilimia 5. Aina ya MT yaliyokuwa mengi ni kuarifu ambayo yalikuwa 6 yakiwa ni asilimia 29. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ndiyo iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kukaribisha yakiwa ni 4 ambayo ni asilimia 67. Riwaya ya *Ndoto ya Almasi* haikuwa na tamko lolote la kuarifu. Aina ya pili katika idadi ya juu katika MTT yalikuwa matamko ya kudai yakiwa 5 ambayo ni asilimia 24. Riwaya iliyokuwa na idadi ya juu ya matamko ya kudai ni *Ndoto ya Almasi* 3 ambayo ni asilimia 60 na *Kidagaa Kimemwozea* yakiwa ni 2 ambayo ni asilimia 40. Kwa mfano,

***Kidagaa Kimemwozea*: MTT:09** *Kwa mara nyingine leo nimethibitisha kwamba mswada huu ulikubaliwa na kuchapishwa japo uandishi ukapewa mwingine.* Uk 141
Amani yuko kibandani mwa Majisifu akisaidiwa na Imani. Baada ya kusoma nakala ya riwaya aliyopewa na Majisifu, anamwandikia Imani kwa vile hakuweza kuongea. Anamweleza jinsi ambavyo amethibitisha kwamba mswada ule alitumbukiza majini kumbe ulichapishwa na jina la mwandishi likawa Majisifu. Mswada wa Amani ulikataliwa na Majisifu kwamba haichapishiki kumbe ulichapishwa. Hali ilivyo ulimwenguni ni kwamba *Kidagaa Kimemwozea* ilichapishwa na inavuma sana. Kiwango cha kuthibitisha ukweli au uongo kiko juu. Mashaka anasema riwaya hiyo imempa jina na umaarufu Mwalimu Majisifu ilhali wanafunzi wa vyuo vikuu wanamwuliza ikiwa yeye ndiye mwandishi kweli. Amani anamweleza Imani kuwa amethibitisha mwizi wa mawazo yake yaani mswada.

***Siku Njema*: MTH: 14***"Usinishukuru mimi wala kunisifu," nikamweleza. " mshukuru na kumsifu Rabi aliyekupa wewe utambuzi wa kutambua hatari iliyokukabili."*
*Amina alinitazama kama atazamaye sinema ya kupendeza ajabu.* Uk 80
Tamko limetolewa na Kongowea. Wakiwa njiani wakati wa mazishi ya Rashid yalipokuwa yanatayarishwa na marafiki zake kama Kongowea. Amina alikuwa ameonywa na Kongowea kuwa aache kuuza mwili wake. Alibadili sera yake ya maisha na kuacha ndiposa anamshukuru Kongowea kwa kumsaidia kutambua hatari iliyomkumba. Msemaji anaeleza kuwa aliyemsaidia kutambua hatari hiyo ni Mungu. Shukrani zimwendee yeye. MT hapa ni kueleza kuwa Kongowea hakuwa na uwezo wa kumtoa Amina katika ukahaba lakini ni Mungu.

**MAHITIMISHO NA PENDEKEZO**
**Mahitimisho:** Makala ilibaini kuwa MT yaliweza kudhihirishwa kulingana na sifa za muanisho wa Searle (1986). Makala ilibainisha aina tano za MT kwa kutumia vigezo vya Searle vya VUI na kugawa aina hizi katika makundi mengine au aina yake tofautofauti, kisha kuthibitisha kwa mifano ya matamko katika riwaya. Makala ilibaini MT 285 katika riwaya zilizoteuliwa. Makala iligundua kuwa kila aina ya MT hutamkwa na msemaji akiwa na maana fulani dhamirifu akilini. Uchanganuzi ulifanywa ili kueleza namna msemewa alivyofasiri tamko. Makala iligundua kuwa MTE yalikuwa mengi 121 kwa 285 kumaanisha wahusika walidhamiria kusababisha wasemewa kutekeleza mambo fulani fulani kwa wakati ujao na tendo liwe la hiari. Idadi kubwa ya MTE ilikuwa matamko ya kuamuru. Hii inamaanisha kuwa kuwa msemaji alitumia mamlaka aliyo nayo kushurutisha msemewa atende jambo kwa kuzingatia kanuni ya kiilokusheni. Kanuni ya uaminifu ni kuwa M alikuwa na imani kwamba W ana uwezo wa kutekeleza kitendo na tamko lichukuliwe kuwa amri. Matamko mengine mengi yalikuwa ya kukaribisha. Hiyo ina maana kuwa wasemaji walifurahia au walikuwa na nia njema kwa

wasikilizaji. Ni muhimu kuchunguza namna watunzi hutumia lugha wanapoandika kazi zao. Nadharia ya VU hutupatia njia ya kuzungumza kuhusu tamko kwa kurejelea sifa zake za nje za kisarufi, muktadha wake, nia, mtazamo wa msemaji na matarajio ya washiriki, uhusiano baina yao pamoja na kanuni na kaida zisizotajwa zinazojitokeza wakati wa kutamkwa na kupokelewa (Pratt, 1977). Makala hii imethibitisha makisio kuwa uchanganuzi wa kipragmatiki wa VU unaweza kuwa na umuhimu katika usomaji, uchanganuzi na ufasiriaji wa mazungumzo ya wahusika na maana anayonuia mwandishi wa riwaya.

**Pendekezo:** Makala hii ilibainisha kwamba nadharia ya kiisimu inaweza kutumika kuchanganua matini ya kifasihi. Utanzu wa fasihi uliochunguzwa ulikuwa ni riwaya hivyo basi, mtafiti anapendekeza tafiti zaidi zifanywe katika tanzu nyingine za fasihi kama tamthilia na hadithi fupi.

**MAREJELEO**


Akinkurolere, S. O., & Ariyo, K. S. (2015). Speech acts features of select extracts in Chinua Achebe's *Arrow of God*. *British Journal of Education, Society and Behavioural Science, 9*(2), 139–145.

Austin, J. L. (1962). *How to do things with words*. Oxford University Press.

Bach, K., & Harnish, R. M. (1979). *Linguistic communication and speech acts*. MIT Press.

Bennett, A., & Royle, N. (1995). *An introduction to literature, criticism and theory*. Longman.

Blakemore, D. (1992). *Understanding utterances: An introduction to pragmatics*. Blackwell.

Bussmann, H. (1996). *A dictionary of language and linguistics*. Routledge.

Harnish, R. M. (2007). *Performative utterances: Seven puzzles*. MIT Press.

Huang, Y. (2009). Speech acts. In J. L. Mey (Ed.), *A concise encyclopedia of pragmatics* (2nd ed., pp. 1000–1009). Elsevier.

Kaburise, P. (2011). *Speech act theory and communication: A Univen study*. Cambridge Scholars Publishing.

Kyeu, D. (2014). *Nadharia ya kitendoneni na jinsi inavyoweza kutumika kuchanganua usemi* (Unpublished thesis).

Leech, G. (1983). *Principles of pragmatics*. Longman.

Levinson, S. C. (1983). *Pragmatics*. Cambridge University Press.

Lyons, J. (1977). *Semantics* (Vols. 1–2). Cambridge University Press.

Malik, F. (1995). *Performance utterances: Their basic and secondary meanings with reference to five English translations of the meanings of the Holy Quran* (Unpublished doctoral dissertation). Durham University.

Matthews, P. H. (2007). *The concise dictionary of linguistics* (2nd ed.). Oxford University Press.

Nyangeri, N. (2014). *Vitendo usemi na ulinganifu wa maana katika tafsiri: Mifano kutoka kazi mbili teule za Barbara Kimenye* (Unpublished thesis).

Oloo, N. O. (2019). *An analysis of speech acts in Margaret Ogola's The River and the Source and I Swear by Apollo* (Unpublished doctoral dissertation).

Patte, D. (1988). Speech act theory and biblical exegesis. In H. White (Ed.), *Speech act theory and biblical criticism (Semeia 41)* (pp. 85–102).

Pratt, M. L. (1977). *Towards a speech act theory of literary discourse*. Indiana University Press.

Sadock, J. K. (1974). *Towards a linguistic theory of speech acts*. Academic Press.

Searle, J. (1969). *Speech acts: An essay in the philosophy of language*. Cambridge University Press.

Searle, J. R. (1986). *Expression and meaning: Studies in the theory of speech acts*. Cambridge University Press.

Searle, J. R. (1989). How performatives work. *Linguistics and Philosophy, 12*(5), 535–558.

Umar, T. F. (2016). *The analysis of speech acts of President Joko Widodo at APEC forum* (Unpublished master's thesis).

Walibora, K. (1996). *Siku njema*. Longhorn Publishers.

Walibora, K. (2003). *Kufa kuzikana*. Longhorn Publishers.

Walibora, K. (2006). *Ndoto ya almasi*. Moran Publishers.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa kimemwozea*. Spotlight Publishers.

Wunderlich, D. (1980). Methodological remarks on speech act theory. In J. Searle, F. Kiefer, & M. Bierwisch (Eds.), *Speech act theory and pragmatics* (pp. 291–312).
Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford University Press.